

**Learning by Ear 2009
Children's Rights Series
07 Child exploitation**

Subject: Exploited children (prostitution, slaves...)

Author: Henri Fosto (Cameroon)

Editor: Sandrine Blanchard

Translation: Anne Thomas

Kiswaheli Eric Ponda

	Women	Men	Age	Language
IN/OUTRO	X		Unimportant	
Narrator		X	Ca. 25	
Jules Marcel		X	16	French
Sandrine	X		16	English
Mary	X		16	French
Bertha	X		Adult	English
Xavier		X	Adult	French

!!!! The sound quality is somewhat wanting (stereo problems, sometimes saturated and compressed) !!!!

LbE soundtrack

INTRO:

Hujambo msikilizaji mahali popote ulipo na karibu kwa makala ya saba katika mfululizo huu wa vipindi vya ‘Noa” Bongo Jenga Maisha yako” kuhusu maswala ya Haki za watoto na juhudi za kuleta Amani. Leo tunafunga safari hadi nchini Cameroon. Mada yetu leo inahusu watoto wanaolazimishwa kuingia katika utumwa – utumwa wa kiuchumi na kimapenzi.

Report

1. Atmo Roundabout 1’36

Narrator:

Tuko katika eneo la biashara la Akwa, mjini Douala, mji mkuu wa kiuchumi nchini Cameroon. Tumefika katika kituo cha Rue de Pau,- moja wapo ya matawi ya Wakfu wa Elimu na Maendeleo ya Watoto nchini Cameroon, ‘FEED’. Shirika hili limeanzisha kituo hiki kwa lengo la kuwasaidia watoto maskini kupata elimu na mafunzo mengine ya taaluma. Tunakutana na Marie Josée aliyelizaliwa mwaka 1992. Hakubahatika kumuona babake na pia mamake alifariki alipokuwa na

umri wa miaka 13 .Tangu wakati huo maisha yake yamekuwa ya taabu na kubahatisha.

2. Marie-José (French)

0'30

"Wakati Mama alipofariki, Mwanamke mmoja alikuja kunichukua kutoka kijijini. Aliniahidi kwamba atanisadia katika masomo yangu. Lakini wakati Mumewe alipofariki pia afya yake ilianza kudhoofika na kuwa mgonjwa sana. Baada ya kusoma kwa mwaka mmoja alinipeleka kufanya kazi katika mkahawa mmoja mjini. Sikuwa nikilipwa mshahara wowote ila nilitegemea bakshishi kutoka kwa wateja wangu."

Narrator:

Marie-José alilazimika kutafuta njia nyingine za kujipatia pesa. Siku moja wakati wa usiku, rafiki yake alimshawishi waandamane hadi barabara ya **Rue de la Joie**, yaani barabara ya raha. Katika barabara hii walijibanza katika mkahawa mmoja, na hapo mara moja Marie-José akafahamu kilichomleta mahala pale. Marafiki hao wawili walianza kuwa na mazoea ya kwenda mahala pale kila siku.

3. Marie-José (French)

0'23

"Nilianza mazoea ya kwenda katika barabara hii nikiwa na umri wa miaka 15. Nilikuwa nikienda mahala hapa kila wakati nilipohitaji pesa. Nilikuwa nikienda kulala na wanaume walionipa pesa katika moja wapo ya vyumba vilivyoko karibu. Na iwapo alikuwa na pesa nyingi tungeponda raha kwanza usiku kucha au kuandamana naye hadi

nyumbani kwake. Kulikuwa na mwanamume mmoja aliyenialika nyumbani kwake kila baada ya siku mbili au tatu.

Narrator:

Miaka miwili baadaye, Marie-José alijifungua mtoto wa kike baada ya kupata mimba na mmoja wa wateja wake wa kimapenzi. Kinyume na ilivyo desturi kwa wasichana wengi makahaba, ambao hutupa watoto wao wanapojifungua, yeye aliamua kumlea binti yake, labda baada ya kupata habari kuhusu shirika la msaada la FEED.

4. Marie-José (French) 0'14

"Nilipokuwa na mimba ya binti yangu, nilisikia kupitia redio kwamba kuna shirika linalowahudumia watoto yatima. Na kwa kuwa mimi pia nilikuwa yatima, nilidadisi kuhusu shirika hili na hatimaye kuja hapa kujifunza biashara."

5. Atmo keyboard => from ADAMO

6. Marie-José (French) 0'05

"Nataka kuwa mtaalam wa masuala ya Teknolojia ya habari na mawasiliano. Na Mungu akipenda, siku moja nitaweza kuanzisha biashara yangu mwenyewe."

Narrator:

Marie-José alikuwa na chaguo miongoni mwa taaluma mbalimbali zilizokuwa zikitolewa chuoni humo. Teknolojia ya mawasiliano, kozi ya masuala ya nywele, kushona, mafundi wa umeme na Umakanika.

7. Atmo street	0'51
-----------------------	-------------

Narrator:

Tuko katika barabara ya Ndokoti, kuelekea PK12, umbali wa kilomita 12 hivi mashariki mwa katikati ya jiji. Hapa pia shirika hili la FEED limejenga kituo cha watoto yatima. Ni mwendo wa saa 11 na Jengo ni tupu kwani tayari watoto wameenda nyumbani. Hivyo tunalazimika kutembea umbali wa dakika10 kumtafuta Guilène, msichana mdogo anayeangaliwa na shirika lisilo la kiserikali la FEED.

8. Atmo cleaning	0'21
-------------------------	-------------

Narrator:

Tunakutana na Guilène akiwa anfanya usafi. Ana nywele fupi na amevalia rinda la rangi ya waridi. Anaonekana mdogo zaidi kuliko umri wake. Na mwakilishi wa shirika hili anamweleza kwamba madhumuni ya ziara yetu ni kutaka kufanya mahojiano naye., na hapo anaanza kulia.

Mamake alifariki kutokana na ugonjwa wa Ukimwi na hakubahatika kumuona babake. Anazungumza huku akisita sita anapoanza kutueleza

masaibu aliyopitia. Kwamba wakati alipokuwa akiishi na shangazi yake alihujumiwa na mjombake.

9. Guilène (French) 0'23

"Siku moja nilikuwa nikifanya kazi zangu nyumbani, na yeye alikuwa amelala hapo. Kisha ghafla akanishika na kunitisha kwa panga endapo ningepiga makelele. Nikamwambia mimi sitaki lakini akaendelea kunibaka. Nawashauri wasichana wa rika langu wajichunge sana."

Narrator:

Mjombake mwengine kwa jina Victor, alimchukua na kuanza kuishi naye. Kisha Victor akaneda kuripoti kisa hicho kwa maafisa wa Polisi

SKIP O-Tone 10 + narrator text => Go DIRECTLY TO Atmo 11

10. Victor!!! Stereo problem!!! (French) 0'35

Alipofika nyumbani huyu mzee alimlazimisha kuvua nguo. Kulingana na taarifa ya msichana huyo, mjombake alikuwa na panga na alimtisha kumuua endapo angepiga mayowe. Kwanza alimweka vidole kwenye sehemu zake za siri, kisha kutoa ulimi na kuramba ramba matiti kabla ya kutoa uume wake na kumbaka."

Narrator:

Majirani walisikia Guilène akilia na kwenda kumsaidia kabla ya kumfahamisha Victor. Mbakaji huyo sasa anatumika kifungo gerezani.

11. Atmo traffic 1'36

Narrator:

Sasa tuko katika makao makuu ya Asseja. Shirika hili limejitolea kuwasaidia watoto na mabarobaro wanaokumbwa na hali ngumu ya maisha katika mji mkuu wa Cameroon, Yaoundé. Na hapa tunakutana na Jules Marcel.

12. Jules Marcel (French) 0'14

"Naitwa Jules Marcel. Nina umri wa miaka 16. Mamangu alinitupa katika pipa la takataka baada ya kunizaa, na kisha baadaye nikaokolewa na watawa. Nilipokuwa na umri wa miaka saba hivi, waliniuza kwa Mwanamume mmoja kwa kiasi cha faranga 500,000 (yuro 760 hivi.)."

Narrator:

Siku moja, Jules Marcel aliugua. Bosi wake alimuuza kwa tajiri mwengine ambayo kijana huyo alitumikia hadi tajiri huyo alipokufa. Warithi wa Jules Marcel waliamua kutoendelea kumtumikisha.

13. Jules Marcel (French) 0'19

"Kwanza nilikuwa nikiishi barabarani kwa miezi miwili. Nililala nje kwa baridi kali. Nilikuwa nikilala tu. Siku moja tajiri mmoja ambaye ni chifu wa kijiji hicho alikuja kunichukua na kunifanya mtumwa wake. Sikuwa na wakati wa kupumzika. Nilifanya kazi kuanzia saa 12 asubuhi hadi saa 5 usiku. Singeweza kulala hadi kila mmoja katika nyumba hiyo awe amelala. Ilinibidi kuwa macho kwa muda mrefu kwani pia nilikuwa mlinzi wa usiku mlangoni."

Narrator:

Jules Marcel aliokolewa na shirika moja lisilo la kiserikali baada ya mhudumu mmoja wa shirika hilo kumuonea huruma kwa jinsi alivyokuwa akifanyishwa kazi.

14. Atmo Welcome song 0'13

Narrator:

Ushahidi wa kuteswa kwa watoto bado ni dhahiri hasa katika eneo la Bali, kaskazini mashariki mwa Cameroon ambako lugha ya Kiingereza inazungumzwa. Sandrine mwenye umri wa miaka 16 amembeba mtoto mikononi mwake. Licha ya kwamba ni mtoto wake msichana huyu hawezi kusema kwa hakika babake ni nani. Alipokuwa msichana mdogo alifanya kazi ya nyumbani kwa Mama mmoja. Alikuwa akifanya kazi na

kusoma pia. Baada ya kumaliza shule muajiri wake alimuamuru kufanya kazi. Wakati huo Sandrine alikuwa na umri wa miaka 10.

15. Sandrine (English)

0'39

"Niliamka asubuhi na mapema mwendo wa saa 11 hivi, kuosha nyumba, kutayarisha kiamsha kinywa na kisha kuwapeleka watoto shuleni mwendo wa saa mbili asubuhi. Pia nilikuwa nikifanya biashara ya kuuza supu, chakula na kisha kufanya kazi za shambani. Nilifua na kuhakikisha kuwa Mzee amekula kabla ya kwenda kuwachukua watoto shuleni. Muajiri wangu alikuwa amemuahidi Mamangu kwamba atanilipa mshahara lakini hakufanya hivyo. Mwishowe aliniambia nijitafutie chakula, na ndipo nikaanza kurandaranda na kupata mimba ya mtoto niliye naye. Na kisha akanifukuza."

Narrator:

Aliporudi kijijini, Sandrine alijiunga na kituo kimoja cha shirika la Nkumu Fed Fed. Hapa vijana hupewa mafunzo mbali na kupata ushauri kupitia muziki ili kusahau waliyopitia.

16. Atmo percussion

0'41

Narrator:

Unyanyasaji wa kimapenzi na kiuchumi miongoni mwa watoto si jambo geni. Lakini hali hii inazidi kuongezeka nchini Cameroon kutokana na

kuongezeka kwa kiwango cha umaskini. Bertha Titanji ni mshirikishi wa kituo cha N'Kumu cha shirika la Fed Fed. Anasema kwamba baadhi ya wazazi maskini wameanza kuwauza watoto wao kwa matajiri wanaotoa pesa nyingi zaidi baadala ya kuwapeleka kwa jamaa zao kama ilivyokuwa zamani.

17. Bertha (English)

0'06

Huwatumia watoto kwa njia zote, kuwanyanyasa na kisha kuwapokonya pesa zote.

Narrator:

Leo hii kuna zaidi ya watoto 6,000 – wengi wao ni waathiriwa wa unyanyasaji wa kimapenzi ambao wameokolewa na mashirika yasiyo ya kiserikali na taasisi nyingine kama vile shirika la kimataifa la kazi, ILO, ubalozi wa Marekani na serikali ya Cameroon.

Ili kukomesha udhalimu huu na kuwasaidia vijana walioathirika, mashirika yasiyo ya kiserikali yanawaonya viongozi wa serikali na kubadili maoni ya umma. Hivi ndivyo shirika la Asseja, linavyofanya Xavier Zingui ni katibu mkuu wa shirika hilo. Anaeleza kwamba shirika lake hufanya kazi katika awamu tatu. Kwanza kuwatambua vijana walioathirika kuwapa mafunzo ya taaluma mbalimbali na kisha kuwasaidia kutangamana tena na jamii.

18. Xavier Zingui (French) 0'22

"Hii ina maana kuwa watoto hawa wamejifunza mambo fulani. Baada ya kukamilisha masomo yao wanaweza kutumia ujuzi waliopata kusaidia familia zao. Lakini hapa hatuwezi kusema kuwa tumefaulu au kufikia lengo letu. Kwani huwa hatukomei hapo, hufuatilia shughuli zao kuhakikisha kuwa wanaimarika na kurejea katika maisha yao ya kawaida kataika sehemu walizokokota."

Narrator:

Licha ya juhudi za mashirika haya, visa vya unyanyasaji na ukahaba miongoni mwa watoto vinaendelea kuongezeka nchini Cameroon. Makao makuu ya shirika la kimataifa la kazi, ILO. katika eneo la Afrika ya Kati limechapisha ripoti inayoonyesha kwamba watoto wengi,- wavulana kwa wasichana hutoroka kupitia baharini hadi Africa Magharibi na kuingia nchini Gabon au Guinea ya Ikweta kutafuta ajira.

Mara kwa mara kumetokea visa vya kuzama kwa meli zinazosafirisha watoto kinyume cha sheria katika pwani ya Cameroon. Biashara hii inaonekana kunawiri nchini Cameroon. Kuna idadi kubwa ya watoto kutoka Cameroon na hata mataifa mengine ya kigeni, wengi wao waathiriwa wa visa vya ubakaji na unyanyasaji baada ya kutumiwa kama Watumwa katika mashamba makubwa makubwa, maduka na wengine kama watumishi wa nyumbani. Kazi hizi huathiri malezi ya watoto hao, afya, maendeleo na ukuaji wao kiakili wanapokuwa watu wazima.

End music

OUTRO :

Na hadi hapo ndipo tunapofika mwisho wa kipindi cha leo. Ripoti ya leo imeandikwa na Henri Fotso kutoka nchini Cameroon. Ukipenda kukisikiliza tena kipindi hik temebela mtandao, tovuti yetu ni: www.dw-world.de/lbe. Hadi wakati mwengine kwaheri!

End music

END